Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

HEET
HIGHER EDUCATION FOR ECONOMIC TRANSFORMATION

HEKIMA NI UHURU

Toleo la 05

# Jarida la HEET UDSM

Toleo la Aprili - Julai 2024

HEET

Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi




**Ujenzi wa Majengo 21 ya Kisasa UDSM Waanza...** Uk 6



**Meneja wa Benki ya Dunia Atembelea UDSM...** Uk 5



**UDSM Yafanya Ziara ya Ulinganishi Viwango...** Uk 8

## Katika toleo hili...


**Mchakato wa Mapitio** *ya Programu 222 UDSM Wakamilika* 15

**Mkakati ya Kuzuia Ukatili** *wa Kijinsia Waimarishwa Kupitia Mradi wa HEET* 17

**Mwongozo wa Kushughulikia** *Malalamiko Maeneo ya Ujenzi Waandaliwa* 18

**UDSM Chapiga Hatua Kubwa** *Utekelezaji wa Mradi wa HEET* 20

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| 3 | Salamu za Makamu Mkuu wa Chuo |
| 4 | Ujumbe wa Mratibu |
| 5 | Meneja wa Benki ya Dunia Apongeza Maendeleo ya Mradi wa HEET- UDSM |
| 6 | Ujenzi wa Majengo 21 ya Kisasa UDSM Waanza |
| 8 | Mkakati wa Kukipaisha Chuo Wafanyika Kupitia Ziara ya Ulinganishi Viwango |
| 10 | Ujumbe wa Naibu Mratibu |
| 11 | Tahariri |
| 12 | Matukio katika Picha |
| 15 | Mkakati wa Kuzuia Ukatili wa Kijinsia Waimarishwa Kupitia Mradi wa HEET |
| 16 | Mradi wa HEET Wafanikisha Kupatikana kwa Vifaa vya Kisasa vya Mawasiliano UDSM |
| 17 | Mchakato wa Mapitio ya Programu 222 UDSM Wakamilika |
| 18 | Mwongozo wa Kushughulikia Malalamiko Maeneo ya Ujenzi Waandaliwa |
| 20 | UDSM Chapiga Hatua Kubwa Utekelezaji wa Mradi wa HEET |
| 22 | Mnufaika Mwingine Kupitia Mradi wa HEET- UDSM Ahitimu Masomo ya Umahiri |

# Salamu za Makamu Mkuu wa Chuo



## Prof. William A. L. Anangisye

## Makamu Mkuu wa Chuo

Ninatumia fursa hii kwa mara nyingine kuwakaribisha tena wasomaji wetu katika toleo la tano la Jarida la HEET-UDSM. Tunafurahi kuona kwamba tunatimiza miezi 20 ya utekelezaji wa Mradi huu kwa mafanikio makubwa. Menejimenti ya Chuo na timu ya utekelezaji wa Mradi inaahidi kuharakisha kasi ya utekelezaji wa Mradi ili kuhakikisha kwamba malengo yake yanafikiwa kwa ubora na ufanisi uliokusudiwa.

Jarida hili linatumika kama njia ya kuwashirikisha wadau kuhusu utekelezaji na maendeleo ya Mradi wa HEET. Aidha, tumekuwa tukifanya mikutano kadhaa na wadau, kutoa taarifa kwa umma, na kuvishirikisha vyombo vya habari na wanahabari kwa lengo la kusambaza habari kwa njia mbalimbali, ili kuhakikisha kuwa jamii inakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu maendeleo ya Mradi wa HEET-UDSM.

Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo ya Mradi wa HEET unawianishwa na mipango mikakati mbalimbali ya Chuo inayoendana pia na vipaumbele vya kimkakati vya taifa. Aidha, mpango mkakati wa uwekezaji wa Chuo umeandaliwa kwa namna ambayo unafanikisha utekelezaji wa Dira ya UDSM ya mwaka 2061 na mpango mkakati wa miaka mitano 2020/2021-2024/2025 (uliorekebishwa). Kwa hakika, kuwekeza kwa wanafunzi, wafanyakazi na jamii ni kipaumbele muhimu kwa Chuo.

Ni vyema kutambua kwamba, Chuo kimeendelea na ufuatiliaji na tathmini ya Mradi ili kuhakikisha mafanikio katika malengo ya maendeleo ya Mradi yaliyowekwa, yanatekelezwa. Tangu toleo la mwisho la Jarida hili, Chuo kimefanya mipango kadhaa ya kimkakati ambayo imeleta matokeo chanya. Aidha, Chuo kimeimarisha timu ya ufuatiliaji na tathmini ili kuakisi hatua ya sasa ya utekelezaji wa Mradi. Ili kufanikisha hili, Mwongozo wa Utaratibu wa Kushughulikia Malalamiko umeandaliwa na umeanza kutumika wakati mpango endelevu wa Mradi ukiendelea kutekelezwa.

Menejimenti inalenga kuhakikisha kuwa angalau 45% ya fedha za Mradi zinapatikana; na kwa wakati wa tathmini ya kati ya Mradi, tunatarajia kuwa tumefikia malengo kwa 60%. Hivi sasa, wakandarasi wamekabidhiwa maeneo kumi kati ya kumi na moja ya ujenzi. Eneo moja lililobaki litakabidhiwa hivi karibuni mara baada ya taratibu za ununuzi kukamilika.

Menejimenti inakipongeza kwa dhati Kitengo cha Utekelezaji wa Mradi kwa jitihada zake za kuhakikisha kwamba Mradi unatekelezwa kwa wakati na kwa ufanisi wa hali ya juu. Ninatoa wito kwa wakandarasi na washauri wa Mradi kuhakikisha kwamba wanatekeleza majukumu yao huku wakizingatia masharti yote yaliyomo katika mikataba yao, huku wakiweka mbele maslahi ya taifa.

Utekelezaji wa shughuli zinazohusiana na mitaala kama vile ulinganishi viwango, mapitio ya mtaala, ushirikiano na tasnia mbalimbali na mpango wa kuzingatia mbinu bunifu katika ufundishaji uko katika hatua nzuri na unatia matumaini sana. Menejimenti ya Chuo itahakikisha kwamba malengo ya mchakato wa mapitio ya mitaala, utekelezaji wa mpango wa kuwa na kampasi maizi na wanufaika wa Mradi wa HEET kumaliza masomo yao kwa wakati yanafikiwa kama yalivyopangwa.

Ninatumia fursa hii kuwashukuru wadau wote ambao wameendelea kuwa msaada kwetu katika utekelezaji wa Mradi wa HEET-UDSM. Menejimenti inatambua na kuthamini msaada inaoendelea kuupata kutoka kwa Serikali, Benki ya Dunia, jamii na vyombo vya habari. Tunathamini pia ushirikiano ambao tumeendelea kuupata kutoka kwa wadau mbalimbali katika utekelezaji wa Mradi wa HEET, kwani mafanikio yetu mbali na mambo mengine, yametokana na mafunzo tuliyoyapata kutoka kwa wadau wetu. Chuo kinawahakikishia wadau wote kuwa milango iko wazi wakati wote, siyo tu katika Mradi wa HEET bali pia katika utelezaji wa shughuli zote za kila siku.

Kwa mara nyingine ninawakaribisha wasomaji nikiamini kwamba mtafurahia kulisoma Jarida hili na kunufaika na maudhui yaliyomo.

# Ujumbe wa Mratibu



**Prof. Bernadeta Killian**

**Mratibu wa Mradi HEET-UDSM**

Karibuni sana wasomaji wetu katika toleo la tano la Jarida la HEET. Katika jarida hili, mbali na mambo mengine, tunapenda kukufahamisheni wasomaji wetu kuhusu hali ya utekelezaji wa shughuli za Mradi wa HEET katika Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Shughuli hizi zimeelekezwa katika maeneo matano ya kipaumbele ambayo ni: Uhandisi na Teknolojia, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Kilimo na Kilimobiashara, Uhandisi wa Miji na Mazingira na Uchumi.

Hatua kubwa iliyofikiwa katika Mradi ni pamoja na kusainiwa kwa mikataba ya usanifu, mapitio na usimamizi wa shughuli za ujenzi katika maeneo ya Dar es Salaam, Zanzibar na Lindi, tarehe 2 Novemba 2023. Vile vile, tarehe 22 Februari 2024 tulisaini mikataba ya ukarabati wa majengo katika Mkoa wa Dar es Salaam na ujenzi wa majengo mapya katika mikoa ya Dar es Salaam, Zanzibar na Lindi. Tunafurahi kuwajuza kwamba wakandarasi wote waliahidi mbele ya Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, aliyeshuhudia utiaji saini wa mikataba hii, kwamba, watakamilisha shughuli za ujenzi kabla au ndani ya kipindi cha miezi 18 kama ilivyopangwa. Mkataba wa ujenzi wa majengo ya Kampasi ya Kagera unatarajiwa kusainiwa kabla ya mwisho wa mwezi Aprili 2024 baada ya kukamilika kwa taratibu za ununuzi.

Kwa upande wa uboreshaji wa miundombinu na vifaa vya kujifunzia, kupitia Mradi huo, Chuo kimenunua vitendeakazi kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Aidha, baada ya kukamilika kwa utafiti fuatilizi, takribani programu 222, kati ya hizo 94 zinatoka katika programu za kipaumbele zitakuwa zimepitiwa na kuboreshwa. Hadi sasa programu 185 zimepitiwa, na programu mpya 37 zitaanzishwa. Vilevile, Chuo kimeandaa mwongozo utakaopitiwa na kuidhinishwa kwa ajili ya kuanza kutumika. Mwongozo huu utawaongoza wanataaluma katika utekelezaji wa mitaala iliyopitiwa na kuboreshwa pamoja na programu mpya zitakazoanzishwa.

Aidha, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kupitia Mradi wa HEET, kimeboresha Mfumo wa Majarida Mtandaoni (OJS) hadi toleo la 3.4.0-1. Mfumo huu utaboresha mchakato wa kupokea na kutathmini makala kupitia mfumo wa makala kupokelewa na kutathminiwa kwa ufanisi kwa njia ya OJS. Utekelezaji wa mikataba tisa ya uboreshaji wa miundombinu na vifaa vya kisasa vya TEHAMA kwa kufunga mitandao mipya ya ya TEHAMA, ikiwemo: Core, LAN, na WLAN (Wi-Fi) unaendelea. Mikataba ya usambazaji wa miundombinu na vifaa vya TEHAMA imetiwa saini na vifaa hivyo vinatarajiwa kupokelewa hivi karibuni.

Miongozo minne ya kusaidia kuimarisha ushirikiano wa kiutendaji na tasnia mbalimbali imeandaliwa na kuidhinishwa na Baraza la Chuo. Kamati za Ushauri wa Ushirikiano (IACs) zimeendelea kutekeleza shughuli zake kama ilivyopangwa. Tunafuatilia kwa ukaribu maendeleo ya wafanyakazi 23 ambao wako kwenye mafunzo katika programu za uzamili chini ya ufadhili wa Mradi. Kati ya hao, wafanyakazi watano wamemaliza masomo yao na wamekwisharipoti kazini.

Tunapokaribia kufika katikati ya mwaka wa 2024 na kuingia katika hatua muhimu katika utekelezaji wa Mradi wa HEET, tunatoa wito kwa wasomaji wetu wote; wafanyakazi, wanafunzi na wadau wengine kuendelea kukisaidia Chuo ili kuhakikisha kwamba Mradi huu unatekelezwa kwa ufanisi.

# Meneja wa Benki ya Dunia Apongeza Maendeleo ya Mradi wa HEET- UDSM

*Na Dotto Kuhenga, HEET-UDSM*






Bi. Muna Salih Meky, Meneja Utekelezaji wa Benki ya Dunia, alipotembelea Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM)

Meneja Utekelezaji wa Benki ya Dunia, Bi. Muna Salih Meky amekitembelea Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na kupongeza hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Mradi wa HEET.

Bi. Meky, ambaye alitembelea UDSM tarehe 18 Machi 2024, na kufanya mazungumzo na Menejimenti ya Chuo, wajumbe wa Kitengo cha Utekelezaji wa Mradi, na wadau mbalimbali wa UDSM, kutoka katika tasnia mbalimbali, amekipongeza Chuo kwa kupata maendeleo makubwa katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Mradi wa HEET kwa ufadhili wa Benki ya Dunia.

"Shughuli mbalimbali mnazofanya, na mafanikio yaliyofikiwa vinadhihirisha kiwango cha umakini na jitihada zilizowekwa kwenye mradi huu. Yote haya yanapaswa kuakisiwa katika mpango endelevu ambao utahakikisha mwendelezo baada ya kukamilika kwa mradi huu", amesema Bi. Meky.

Aidha, amekitaka Chuo kufikiria kuongeza jitihada na rasilimali zaidi katika teknolojia ya habari na mawasiliano na teknolojia ya uhandisi ambazo zinashughulikia moja kwa moja mahitaji ya viwanda vya uzalishaji na teknolojia ya kisasa katika ulimwengu tulionao.

Wakati huohuo, Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. William A. L. Anangisye, amesema Chuo kimejipanga kutekeleza Mradi wa HEET na kuzitumia ipasavyo Dola za Marekani milioni 47.5 ambazo zimetengwa kwa UDSM chini ya Mradi huu kwa kipindi cha miaka mitano (2021-2026).

Prof. Anangisye ameendelea kueleza kwamba, shughuli mbalimbali zimetekelezwa chini ya maeneo matano ya kipaumbele katika Mradi huo ambayo ni: Uhandisi na Teknolojia, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Kilimo na Kilimobiashara, Uhandisi wa Miji, Mazingira na Uchumi.

"Tangu kuanza kwa Mradi mwezi Agosti, 2022 hatua kadhaa zimefikiwa. Kwa upande wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu, majengo 24 ambayo yatatumika kama kumbi za mihadhara, ofisi, maabara, karakana, studio, na hosteli yanajengwa", amesema Prof. Anangisye.

Prof. Anangisye ameeleza pia kwamba, shughuli za uendelezaji wa miundombinu kupitia Mradi wa HEET ni pamoja na uanzishwaji wa kampasi mpya katika mikoa ya Lindi na Kagera kwa ajili ya kilimo na biashara mtawalia. Majengo zaidi yamepangwa kujengwa katika Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere- Mlimani, zikiwemo, Kunduchi, Kijitonyama na Buyu, Zanzibar.

"Mikataba ya mapitio na usimamizi wa shughuli za ujenzi kwa kampasi za Dar es Salaam, Zanzibar na Lindi ulisainiwa Novemba, 2023. Mikataba ya ukarabati wa majengo kwa Dar es Salaam na ujenzi wa majengo mapya kwa Dar es Salaam, Zanzibar na Lindi ilisainiwa Februari, 2024. Ni matumaini yetu kuwa shughuli za ujenzi zitakamilika ndani ya kipindi cha miezi 18 kama ilivyopangwa", amesema Prof. Anangisye.

Ameendelea kufafanua kuwa, mkataba wa ujenzi wa majengo ya Kampasi ya Kagera ulitarajiwa kusainiwa kabla ya mwisho wa mwezi Aprili, 2024 baada ya kukamilika kwa taratibu za ununuzi. "Kwa upande wa uimarishaji wa vifaa na miundombinu ya kujifunzia, Chuo kupitia Mradi wa HEET kimenunua kompyuta na vifaa mbalimbali vya TEHAMA kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu".

Inaendelea Uk. 19...




# Ujenzi wa Majengo 21 ya Kisasa UDSM Waanza

Na Dotto Kuhenga, UDSM-HEET

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kimesaini mikataba na wakandarasi wanne kwa ajili ujenzi wa majengo 21, kati ya 24 yaliyopangwa kujengwa Dar es Salaam, Zanzibar, Lindi (Ngongo na Ruangwa) na Kagera kupitia Mradi wa HEET.

Hafla ya uzinduzi wa ujenzi wa majengo haya ilifanyika tarehe 22 Februari 2024 ambapo mgeni rasmi alikuwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Omary Kipanga (Mb.). Wengine waliohudhuria ni Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, Mhe. Balozi Mwanaidi Sinare Maajar, aliyewakilishwa na Balozi Tuvako Manongi, Rais wa Jumuiya ya Wahitimu, UDSM.

Naibu Waziri, Mhe. Kipanga, ambaye alimwakilisha Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof. Adolf Mkenda, alisema ujenzi wa majengo hayo ni hatua ya kupongezwa kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika utekelezaji wa Mradi wa HEET.

“Ni dhahiri kwamba, fedha nyingi zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa HEET kwa upande wa UDSM; hivyo, Chuo kihakikishe kuwa hadi kufikia Juni 2026, fedha hizi ziwe zimetumika ipasavyo katika kufanikisha malengo ya Mradi”, amesema Mhe. Kipanga.

Ameendelea kueleza kuwa, Wizara imejipanga vyema kuratibu, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Mradi huo. “Mara kwa mara tutaendelea kuwasisitiza kwamba mnahitaji kuharakisha utekelezaji wa Mradi huu, na ikiwa mtapata changamoto yoyote, msisite kushauriana na Wizara ili kuhakikisha Mradi unatekelezwa kwa ufanisi uliokusudiwa”.

Aidha Mhe. Kipanga amewataka wakandarasi waliosaini mikataba hiyo kujenga majengo hayo kwa kuzingatia wajibu wa kisheria na kimaadili huku wakihakikisha kwamba ujenzi huo unakamilika kwa wakati na kwa ufanisi.

Kwa upande wake Mkuu wa Chuo, Dkt. Jakaya Kikwete, amesema kwamba Chuo kimejipanga kuwasimamia kwa ukaribu wakandarasi na washauri wa Mradi ili kuhakikisha kwamba kinafanikiwa katika azma yake ya kuwa na majengo ya kisasa.

Akionekana kufurahishwa na matarajio ya kufanikiwa kwa Mradi huu, Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. William A. L. Anangisye, amesema kwamba, Mradi wa HEET mbali na mambo mengine, umelenga katika kuboresha miundombinu ya Chuo na kununua vifaa vya kisasa, mambo ambayo yanaendana na Dira ya UDSM ya 2061 na mpango mkakati wenye lengo la kuwa na mageuzi makubwa ya kitaasisi kulingana na mahitaji ya sasa na ya baadaye ya maendeleo ya taifa.



## Wakandarasi na Miradi ya Ujenzi

Kwa mujibu wa Prof. Bernadeta Killian, ambaye pia ni Mratibu wa Mradi wa HEET-UDSM na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo- Mipango, Fedha na Utawala, wakandarasi wanne waliosaini mikataba ya kutekeleza miradi hiyo ya ujenzi ni: M/S Mohammed Builders; M/s B.H. Ladwa; M/S Til Construction; na M/s Shandong Hi-Speed.

Amesisitiza kwamba, kwa mujibu wa mkataba huu, ujenzi unapaswa kukamilika katika kipindi cha muda wa miezi 18 tangu tarehe ya kusainiwa kwa mkataba huu, ambapo jumla ya gharama kwa miradi yote ni TZS 45,993,168,271,79.

Mkataba kati ya UDSM na M/S Mohammed Builders unahusisha shughuli za ujenzi katika Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere- Mlimani wenye thamani ya TZS 15,696,130,949,32 ukijumuisha ujenzi wa majengo katika Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia (CoET) wenye thamani ya TZS 9,052,693,573.95 na ujenzi wa bweni la wanafunzi wa uzamili na jengo la Jinsia na watu wenye mahitaji maalum. wenye thamani ya TZS 6,643,437,375.37.

"Ujenzi katika Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia unahusisha ukarabati wa Bloku L, O na Q; ujenzi wa jengo jipya linalojumuisha maabara 7; jengo jipya lenye karakana 5; jengo jipya kwa ajili ya ukumbi 1 wa mihadhara (wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 250), vyumba 3 vya mihadhara (kila kimoja kikiwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 50) na chumba 1 cha studio wa kuchukua wanafunzi 50 wa programu ya usanifu vitambaa), wakati bweni la wanafunzi litakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 51, na jengo la Jinsia na watu wenye mahitaji maalum litatumika kwa ajili ya huduma za masuala ya jinsia na mahitaji maalum.", amesema Prof. Killian.

"Mkataba na M/s B.H. Ladwa, wenye thamani ya TZS 6,459,181,103.97, unahusisha ujenzi wa jengo 1 la mihadhara lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 140; studio 1 ya maltimidia yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 50; maabara 3 za kisasa zitakazokuwa na vifaa vyenye teknolojia ya hali ya juu, kila moja ikiwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 48; na karakana 2, kila moja ikiwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 30 katika Ndaki ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Kijitonyama", amesema Prof. Killian.

Aidha, amesema kuwa kutakuwa na ujenzi wa vyumba 3 vya mihadhara, kila kimoja kikiwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 100 na maabara 1 yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 50 katika Shule ya Kuu ya Sayansi ya Akua na Teknolojia ya Uvuvi iliyopo Kunduchi.

## Majengo ya IMS, Ruangwa na Ngongo

Mkataba kati ya UDSM na M/S Til Construction wenye thamani ya TZS 10,118,405,530.78 unahusisha ujenzi wa majengo mapya 11 yakiwamo ya utawala na taaluma (kwa ajili vyumba vya mihadhara, maabara, ukumbi wa mikutano, ofisi za wafanyakazi na jengo moja jipya la hosteli litakalokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 80 katika Taasisi ya Sayansi za Bahari (IMS) Buyu, Zanzibar.

Prof. Killian ameendelea kueleza kwamba, "mkataba kati ya UDSM na M/s Shandong Hi-Speed wenye thamani ya TZS 13,719,450,687.7 unahusisha ujenzi katika maeneo ya Ruangwa na Ngongo mkoani Lindi".

Amefafanua zaidi kuwa, katika eneo la Ngongo kutajengwa jengo la utawala, jengo la vyumba vya mihadhara (vyenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 360), jengo la maabara, jengo la karakana (vyumba 5), jengo la hosteli za wanafunzi wa kiume na hosteli za wanafunzi wa kike. Katika eneo la Ruangwa, kutakuwa na ujenzi wa ukumbi wa mihadhara (wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 50) na jengo 1 la hosteli ya wanafunzi 56 (wa kike 22 na wanaume 34).

Aidha, Prof. Killian amesisitiza kuwa ujenzi wa majengo hayo 21 unaendana la lengo la HEET la kuboresha mazingira ya kujifunzia kwa kuzingatia mahitaji ya soko la ajira kwa programu za kipaumbele katika vyuo vya elimu ya juu pamoja na kuboresha mfumo wa usimamizi wa elimu ya juu nchini Tanzania.

## Mkataba kwa ajili ya Usimamizi wa Ujenzi katika Kampasi ya Kagera

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pia kilisaini mkataba wa usimamizi wa ujenzi na M/s Mhandisi Consultancy Ltd akishirikiana na M/s MD Consultancy Limited kwa ajili ya majengo matatu katika Kampasi ya Kagera.

Majengo hayo matatu ya kampasi ya Kagera yanayokamilisha jumla ya majengo 24 ya Mradi wa HEET UDSM, yanahusisha jengo la utawala na taaluma, kafeteria, jengo la biashara, na jengo la hosteli za wanafunzi wa kike.



# Mkakati wa Kukipaisha Chuo Wafanyika Kupitia Ziara ya Ulinganishi Viwango

*Na Jackson Isdory, UDSM-HEET*










Viongozi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hivi karibuni wamehitimisha ziara yao ya ulinganishi viwango katika vyuo vikuu vyenye hadhi ya juu ulimwenguni katika mabara ya Afrika, Asia na Ulaya, ikiwa ni mkakati mmojawapo wa kukipaisha Chuo. Ziara hii imefadhiliwa na Mradi wa HEET.

Kwa mujibu wa Dkt. Liberato Haule, Naibu Mratibu wa Mradi wa HEET-UDSM, ziara hii imefanyika kupitia mpango wa ziara ya ulinganishi viwango katika vyuo vikuu vya nchi za Ghana, Afrika Kusini, Korea Kusini, na Ujerumani kwa lengo la kuboresha utendaji wa Chuo ikiwa ni pamoja na mapitio ya mitaala kulingana na mahitaji ya sasa ulimwenguni.

"Kuanzia Mradi huu ulipoanza mwaka 2022, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimeendelea kupokea maoni ya wadau wa ndani na nje kwa lengo la kuboresha mfumo wake wa elimu. Utafiti fuatilizi na mpango wa tathmini binafsi ya kitaasisi, unalenga kubainisha maeneo yenye ubora na fursa kwa lengo la kujiimarisha kitaasisi na kujenga mustakabali mwema wa kitaifa.", amesema Dkt. Haule.

Naye Prof. Masoud Muruke, Mratibu wa Mapitio ya Mitaala, amesisitiza umuhimu wa ziara hii katika kuimarisha utamaduni wa kujenga umahiri. Ulinganishi viwango unatoa fursa ya kipekee kwa Chuo kujifunza kutokana na mafanikio ya vyuo vingine vikubwa duniani ambapo tunaweza kutumia fursa hii kuweka mikakati ya kuboresha mfumo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika utoaji wa elimu ya juu.

## Kujiimarisha katika Mfumo wa Teknolojia na Usawa wa Kijinsia

Timu iliyofanya ziara ya ulinganishi viwango nchini Ghana ilitembelea Chuo Kikuu cha Ghana, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Kwame Nkrumah na Chuo Kikuu cha Cape Coast.

Timu hii iliyoongozwa na Mwanasheria Mkuu na Katibu wa Baraza la Chuo, Prof. Saudin Mwakaje, ilizingatia kwamba vyuo vikuu nchini Ghana vimejiimarisha katika mfumo wa ufundishaji kwa njia ya mtandao, masuala ya utafiti na kujenga muunganiko wa kiubunifu katika matumizi ya akili unde na shughuli za kitaaluma.

Mambo yaliyoshuhudiwa katika vyuo vikuu nchini Ghana yanaonesha namna walivyojiimarisha katika masuala ya usawa wa kijinsia, ambapo mbali na mambo mengine, wanawake wanashika nafasi za juu za uongozi. Hatua hii ya kidemokrasia na kujiimarisha katika mifumo ya kitehama vinavifanya vyuo vikuu vya Ghana kupiga hatua kubwa katika mfumo shirikishi na ubunifu.

Prof. Mwakaje alieleza pia kuwa walivutiwa sana na msisitizo uliowekwa katika ufundishaji kwa njia ya mtandao na matumizi ya akili unde katika mfumo wa elimu, hususani katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Kwame Nkrumah. Taarifa hizi zitaleta manufaa makubwa katika mchakato wetu wa kuimarisha mfumo wa ufundishaji kwa njia ya dijitali, Chuo Kikuu cha Da es Salaam.

Wajumbe wengine waliokuwa katika msafara huu ni: Prof. Beatrice Mkenda (Amidi, Shule Kuu ya Uchumi), Prof. Siasa Mzenzi (Mkurugenzi wa Mipango na Uwekezaji,) na Dkt. Latifa Mbelwa (Amidi, Shule Kuu ya Biashara).

## Kujiimarisha katika Mfumo Jumuishi wa Elimu

Timu nyingine iliyoongozwa na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo-Taaluma, Prof. Bonaventure Rutinwa ilifanya ziara katika vyuo vikuu maarufu nchini Ujerumani ambavyo ni: Chuo Kikuu cha RWTH Aachen, Chuo Kikuu cha Paderborn na Chuo Kikuu cha Constructor.

"Ziara yetu nchini Ujerumani imekuwa chachu katika kujenga mfumo jumuishi wa elimu. Vyuo tulivyovitembelea vimetuimarisha katika kujenga ushirikiano baina ya taaluma anuai. Tunashukuru kwamba tumepanua wigo wa ushirikiano baina ya UDSM na vyuo tulivyovitembelea", amesema Prof. Rutinwa.

"Taasisi tulizozitembelea zinadhihirisha namna ambavyo masuala ya ujumuishi wa taaluma mbalimbali na utafiti yanavyozingatiwa nchini Ujerumani. Mathalani, Chuo Kikuu kikongwe cha RWTH Aachen, kilidhihirisha umahiri wake katika elimu ya uhandisi na teknolojia", amesisitiza Prof. Rutinwa.

Prof. Rutinwa alibainisha pia kwamba vyuo vikuu vilivyotembelewa katika ziara hii kama vile Chuo Kikuu cha Paderborn kinachojulikana kwa falsafa yake shirikishi, kimejenga mazingira mazuri yanayofaa kwa elimu jumuishi. Aidha, Chuo Kikuu cha Constructor, kinachukuliwa kama ngome ya kimataifa ya ukuzaji wa taaluma anuwai, hali inayoonesha dhamira ya dhati ya Ujerumani ya kukuza jumuiya ya kimataifa ya wasomi.

Msafara wa ziara ya Ujerumani pia uliwahusisha Prof. Bakari Mwinyiwiwa (Rasi, Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia), Dkt. Ellen Kalinga (Mhadhiri Mwandamizi, Ndaki ya Habari na Teknolojia ya Mawasiliano), na Dkt. Liberato Haule (Naibu Mratibu- HEET-UDSM).

## Kuimarisha Ubia wa Kimkakati na Ubora wa Kitaaluma

Nchini Afrika Kusini, kulikuwa na msafara ulioongozwa na Prof. Nelson Boniface, Kaimu Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Utafiti, ambao ulitembelea vyuo vikuu vya Pretoria na Rhodes. Katika ziara hiyo, wajumbe walijifunza mwelekeo wa kimkakati wa Afrika Kusini katika kukuza ushirikiano kati ya wasomi, tasnia mbalimbali na serikali ili kuendeleza ubunifu na ubora wa kitaaluma.

Timu hii pia iliwahusisha: Dkt. Egbert Mujuni (Mhadhiri Mwandamizi, Ndaki ya Sayansi Asilia na Tumizi), Dkt. Aurelia Mallya (Mudir, Idara ya Isimu na Lugha za Kigeni, Ndaki ya Insia) na Dkt. Veronica Buchumi (Mhadhiri, Shule Kuu ya Sheria).

Kwa mujibu wa maelezo ya Prof. Boniface, mafunzo yaliyopatikana katika ziara iliyofanywa katika vyuo vikuu vya Afrika kusini hakuna shaka kwamba yatasaidia katika kujenga mustakabali bora wa UDSM. Vyuo vikuu vya Afrika Kusini vinaonesha mfano katika kuyafikia mageuzi ya ushirikiano wa kimkakati baina ya tasnia mbalimbali, serikali na wadau.



Prof. Boniface ameongeza kwamba, vyuo vikuu vya Afrika Kusini vinaonesha ishara bora ya ushirikiano baina ya wasomi na tasnia mbalimbali. Ushirikiano huu unajenga utamaduni wa kukuza ubunifu na ujasiriamali. "Ushirikiano huu ni muhimu sana katika kuandaa wanafunzi kulingana na mahitaji ya soko la ajira", amesema Prof. Boniface.

Kwa upande Dkt. Veronica Buchumi, amesema kwamba msisitizo wa taratibu za tathmini za uwazi na ushirikiano wa sekta mbalimbali nchini Afrika Kusini ni mfano bora wa kuigwa. "Tutazingatia uzoefu huu katika mchakato wa kuboresha mitaala yetu ili kuwaandaa wanafunzi wetu katika taaluma ya sheria.", amesisitiza Dkt. Buchumi.

Aidha, kulikuwa na timu nyingine iliyoelekea Korea Kusini ambayo iliwahusisha Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe, pamoja na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo-Mipango, Fedha na Utawala, Prof. Bernadeta Killian ambayo ilitembelea vyuo mbalimbali nchini Korea ya Kusini vilivyobobea katika teknolojia na nyanja nyingine.

Wajumbe wengine waliokuwa katika timu ya Korea ya Kusini ni: Dkt. Mkabwa Manoko (Rasi, Ndaki ya Sayansi ya Kilimo na Teknolojia ya Chakula) na Dkt. Blandina Lugendo (Amidi, Shule Kuu ya Sayansi Akua na Teknolojia ya Chakula).

## UDSM Kuendelea kuwa Kinara katika Ubora wa Elimu

Kwa mujibu wa Dkt. Haule, mafanikio ya ziara iliyofanywa katika mataifa mbalimbali ni kuweka msingi wa uboreshaji wa kitaasisi, kwa kuzingatia maoni na mikakati itakayopendekezwa na wajumbe walioshiriki ziara hizo.

"Mikakati inayopendekezwa inatokana na mpango mkakati jumuishi na miundo ya utawala iliyo wazi; ushirikiano katika masuala ya teknolojia ya kisasa; kukuza ushirikiano wa sekta mbalimbali; kuwekeza katika maendeleo, motisha kwa wafanyakazi; na kushiriki katika ushirikiano wa kimkakati wa kimataifa", amesema Dkt. Haule.

Amendelea kusema kwamba, kwa kuzingatia mapendekezo hayo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kililenga kuimarisha nafasi yake ya kuwa kinara katika ubora wa kitaaluma duniani katika utoaji wa elimu.

Prof. Bonaventure Rutinwa, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo-Taaluma, alisisitiza umuhimu wa kuzingatiwa kwa mapendekezo yanayotokana na ziara hizi. "Ziara tulizozifanya katika maeneo mbalimbali zimetoa mchango mkubwa na muhimu kutokana na uzoefu wa maeneo mbalimbali ulimwenguni. Ikiwa mafunzo na mapendekezo yaliyotokana na ziara hizi yatazingatiwa, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kitaendelea kuwa kinara katika ubora wa elimu ya juu".

# Ujumbe wa Naibu Mratibu




## Dkt. Liberato Haule

**Naibu Mratibu HEET-UDSM**


Tunayo furaha kuwajulisha wasomaji wetu kuhusu hatua muhimu zilizofikiwa katika utekelezaji wa Mradi wa HEET katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, tangu toleo la mwisho la Jarida hili lilipotoka.

Tumepiga hatua kubwa katika eneo muhimu la ujenzi kwa kusaini mikataba na wakandarasi na kukabidhi maeneo kumi ya ujenzi. Mikataba iliyosainiwa ni ya ukarabati na ujenzi wa majengo katika Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere- Mlimani, Kunduchi, Kijitonyama, Buyu-Zanzibar, Ngongo-Lindi na Ruangwa.

Wakandarasi wamekabidhiwa maeneo ya ujenzi kwa ajili ya kuanza ujenzi. Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Rais mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, aliyeongoza hafla ya utiaji saini ya mkataba huo, aliwasisitizia wakandarasi kuhusu umuhimu wa kukamilika kwa ujenzi ndani ya miezi kumi na minane kama ilivyoainishwa katika mkataba. Aliahidi kufuatilia kwa karibu kila hatua ya ujenzi huo.

Ni dhahiri kwamba kukamilika kwa ukarabati na ujenzi wa majengo katika Mradi huu kutaboresha kwa kiasi kikubwa ufundishaji na ujifunzaji Chuoni. Ukarabati na ujenzi huu utahusisha maeneo mbalimbali ndani na nje ya Dar es Salaam. Katika Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia kutafanyika ukarabati wa bloku L, O na Q; maabara mpya saba, karakana tano mpya, studio moja mpya, ukumbi mmoja wa mihadhara na madarasa yenye uwezo wa kuchukua idadi tofauti ya wanafunzi.

Ndaki ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano itakuwa na jengo moja jipya la ukumbi wa mihadhara, maabara tatu, studio moja na karakana mbili mpya. Aidha, Shule Kuu ya Sayansi ya Akua na Teknolojia ya Uvuvi itakuwa na jengo jipya kwa ajili ya madarasa na maabara.

Majengo zaidi katika Kampasi ya Mwalimu Nyerere Mlimani yatajumuisha hosteli ya wanafunzi wa shahada za uzamili na huduma za jinsia na mahitaji maalumu. Aidha, kukamilika kwa ujenzi katika eneo la Buyu- Zanzibar kutaongeza miundombinu kwa Taasisi ya Sayansi za Bahari kwa upande wa vyumba vya madarasa, maabara za kompyuta, ofisi za wanafunzi wa shahada za uzamili na hosteli za wanafunzi wa kiume na wa kike.

Kampasi mpya za Ngongo na Ruangwa zitahusisha ujenzi wa majengo ya utawala, vyumba vya mihadhara, karakana, maabara, kafteria, na hosteli za wanafunzi wa kiume na wa kike.

Upitiaji wa mitaala pia umefanyika kama lengo mojawapo la Mradi. Kama sehemu ya Mradi, mitaala imeboreshwa kwa kuzingatia mahitaji ya sasa na mbinu za kiubunifu katika ufundishaji. Vitengo vyote vya kitaaluma tayari vimewasilisha mitaala iliyopitiwa, ikiwa ni pamoja na programu mpya zilizoanzishwa ili viweze kutathminiwa na timu iliyoundwa. Mchakato huu uliwashirikisha kikamilifu wadau wa ndani na nje.

Sambamba na uboreshaji wa miundombinu na mapitio ya mitaala, Mradi unalenga pia katika ununuzi wa vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia zitakazofungwa katika majengo mapya yaliyojengwa. Kama ilivyofanyika kwa mapitio ya mitaala, vitengo vya kitaaluma vitakuwa mstari wa mbele katika kubainisha na kuamua aina za vifaa vya kujifunzia kwa kuzingatia mahitaji ya mitaala na rasilimali zilizopo.

Kwa mara nyingine tena, Kitengo cha Utekelezaji wa Programu kinatoa shukurani za dhati kwa jumuiya ya Chuo Kikuu pamoja na wadau wote wa ndani na nje ambao walichangia katika kufanikisha utekelezaji wa Mradi wa HEET na kufikia hatua muhimu zilizoelezwa katika Jarida hili.

# Tahariri

## Usawa na Ujumuishaji wa Kijinsia: Misingi ya Utekelezaji wa Mradi wa HEET

Utekelezaji wa Mradi wa HEET katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, mbali na maeneo mengine unazingatia ujumuishaji na usawa wa kijinsia katika mazingira yote ya kujifunzia na kufundishia. Kwa muktadha huu, kupitia Mradi huu, Chuo kimeweka mipango madhubuti ya kushughulikia tofauti za kijinsia na kuhamasisha ushiriki mkubwa wa wanawake katika taaluma za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM).

Aidha, Chuo kimeandaa mipango ya kuwafikia wanafunzi wa kike wa sekondari; mkakati wa kijinsia wa taasisi ili kuvutia na kudumisha idadi ya wanawake katika programu za kipaumbele, kufuatilia maendeleo yao na kuhakikisha kwamba kunaandaliwa sera na miongozo mbalimbali dhidi ya ukatili wa kijinsia.

Baadhi ya kanuni mpya zilizoundwa kwa ufadhili wa Mradi wa HEET, ni pamoja na: miongozo ya udhibiti wa ukatili wa kijinsia na unyanyasaji wa kingono, miongozo dhidi ya ukatili na unyanyasaji, na miongozo ya kushughulikia malalamiko. Aidha, sera iliyokuwapo ya kupambana na unyanyasaji wa kijinsia imeboreshwa.

Miongozo ya kudhibiti ukatili wa kijinsia na unyanyasaji wa kingono, ukatili na udhalilishaji inalenga kuhakikisha kwamba kunakuwa na mazingira mazuri na huru ya kufanya kazi na kujifunzia, ambayo yanazingatia usawa wa kijinsia na kutokomeza aina zote za ubaguzi, unyonyaji na udhalilishaji wa kijinsia.

Pia, kupitia Mradi wa HEET, Chuo kimeanzisha michakato ya udhibiti wa masuala ya ukatili wa kijinsia kwa kuunganisha na mifumo ya sera ya taifa, kuanzisha programu za ushauri kwa wanawake katika maeneo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati, kujenga hosteli/ mabweni kwa ajili ya wanawake na wanafunzi wenye ulemavu na kuongeza idadi ya uwakilishi wa wanawake kwa upande wa wanataaluma na katika uongozi wa Chuo.

Mradi huo pia umekisaidia Chuo katika uandaaji wa miongozo ya ushughulikiaji wa malalamiko ambayo imeweka kanuni na taratibu za kushughulikia malalamiko Chuoni. Miongozo hii itatumika kama msingi wa taratibu za kushughulikia malalamiko katika ngazi zote za Chuo.

Kwa kuzingatia kuwapo kwa michakato na taratibu hizi zote zinazolenga kuimarisha usawa wa kijinsia na ujumuishaji na kushughulikia masuala ya ukatili wa kijinsia, tunaamini kuwa vitengo vya ufundishaji vya UDSM vitaweza kubainisha na kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalumu kwa kutumia mbinu faafu na rafiki. Aidha, vitengo hivi vinatarajiwa kusisitiza suala la usawa wa kijinsia na ujumuishaji katika maeneo yote.

Hivyo, tunasisitiza kwamba, sera hizi na miongozo inayohusiana na usawa wa kijinsia na ujumuishaji ni muhimu sana kwa jumuiya ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kupitia miongozo hiyo, Chuo kitadumisha sifa yake ya kuwa na mazingira salama na yanayoshughulikia masuala ya kijinsia ya kitaaluma ambapo wadau wote wanachangamana kwa kuaminiana na kuheshimiana na kukifanya Chuo kuwa mazingira yanayojali utu na kuzingatia haki ya utu na usawa wa kijinsia.


### Uratibu wa Mradi wa HEET-UDSM

**Mratibu wa Mradi**
Prof. Bernadeta Killian

**Naibu Mratibu wa Mradi**
Dkt. Liberato V. Haule

### Timu ya Uhariri

**Mhariri Mkuu &**
**Mtaalamu wa Uhusiano kwa Umma na Mawasiliano HEET-UDSM**
Dkt. Dotto Paul Kuhenga

**Wahariri**
Dkt. Lupa Ramadhani (Kiingereza)
Dkt. Mussa Hans (Kiswahili)

**Waandishi:**
Jackson Isdory
Zamda George
Ally Mambele
Mercy Machange
Remmy Wilson

**Mpiga Picha:**
Tumaini Kibangala

**Msanifu**
Michael Mwakatobe




# Matukio katika Picha













# Siku ya Wanawake Duniani



















# Ziara ya Ulinganishi Viwango

## Ghana



Timu ya UDSM iliyotembelea Chuo Kikuu cha Kwame Nkrumah cha Sayansi na Teknolojia, Ghana tarehe 18 Januari 2024. Timu pia ilitembelea Chuo Kikuu cha Ghana na Chuo Kikuu cha Cape Coast. Katika picha kutoka kulia ni Prof. Siasa Mzenzi (Mkurugenzi wa Mipango, Maendeleo na Uwekezaji), Dkt. Latifa Mbelwa (Amidi Shule Kuu ya Biashara), Prof. Beatrice Mkenda (Amidi Shule Kuu ya Uchumi) na Prof. Saudin Mwakaje, Kiongozi wa msafara na Mwanasheria Mkuu wa Chuo na Katibu wa Baraza.




Nembo ya Chuo Kikuu cha Kwame Nkrumah

## Mafunzo kutoka Korea Kusini



Timu ya UDSM ikiwa na mwenyeji wake katika Ndaki ya Kilimo na Sayansi Asilia, Chuo Kikuu cha Taifa cha Seoul.




Prof. James Mdoe (kushoto), Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, na Prof Bernadeta Killian (kulia) Naibu Makamu Mkuu wa Chuo, Mipango, Fedha na Utawala baada ya kusaini Mkataba wa Maridhiano baina ya UDSM na Rais wa Chuo Kikuu cha Korea Aerospace Prof.Hee-young Hurr.



## Ziara ya Ujerumani





Timu ya UDSM, Prof Bakari Mwinyiwiwa (Rasi, CoET), Dkt. Liberato Haule (Naibu Mratibu wa Mradi wa HEET) na Dkt Ellen Kalinga (Mratibu wa Mapitio ya Mitaala, CoICT) wakijadili jambo na wenyeji wao kutoka Kitivo cha Uhandisi Umeme Teknolojia ya Mawasiliano, Chuo Kikuu cha RWTH Aachen.

## Ziara ya Afrika Kusini



Picha ya pamoja katika Chuo Kikuu cha Rhodes. Kutoka kushoto ni Dkt. Egbert Mujuni, Dkt. Aurelia Mallya, Prof. Nelson Boniface, Dkt. Nomakwezi Mzilikazi, Dkt. Veronica Buchumi na Prof. Sizwe Mabizela.

# Mchakato wa Mapitio ya Programu 222 UDSM Wakamilika

Na Zamda George, UDSM-HEET



*Mratibu wa Mradi wa HEET Kitaifa, Dkt. Kenneth Hosea (katikati, waliokaa), Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (UDSM)-Taaluma, Prof. Bonaventure Rutinwa (wa kwanza kushoto, waliokaa), Mratibu wa Ushirikiano wa Taaluma na Sekta katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dkt. Khadija Kweka (kulia, waliokaa) na wadau wengine katika moja ya mikutano ya mradi wa HEET, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hivi karibuni.*




Wakati mchakato wa mapitio ya mtaala katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam unapokaribia kufika hatua za mwisho, takriban programu 222 za kitaaluma zilizopitiwa kwa kuzingatia maoni ya wadau na ulinganishi viwango zimewasilishwa kwa ajili ya kuidhinishwa. Jarida hili linaripoti.

Kwa mujibu wa taarifa zilizomfikia mwandishi kutoka katika vitengo mbalimbali vilivyohusika na mchakato huo, jumla ya programu 222 (zikihusisha programu mpya 37) zimewasilishwa kwa ajili ya kuidhinishwa baada ya mchakato wa mapitio kukamilika. Programu hizi ni za shahada za awali na shahada za uzamili.

"Kati ya programu hizo 222, program 94 zilitoka katika maeneo ya kipaumbele ya Mradi wa HEET ambayo ni: Uhandisi na Teknolojia, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Kilimo na Kilimobiashara, Uhandisi wa Miji na Mazingira, na Uchumi", alibainisha Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. William A. L. Anangisye wakati wa ziara ya mwakilishi wa Benki ya Dunia aliyoifanya UDSM hivi karibuni.

Prof. Anangisye ameendelea kueleza kwamba, mchakato wa mapitio uliwashirikisha kwa kiasi wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na wawakilishi wa tasnia mbalimbali. Alisisitiza namna Chuo kilivyozingatia umuhimu wa kuoanisha programu za kitaaluma na mahitaji halisi ya soko la ajira na jamii kwa ujumla.

"Utafiti huu ulihusisha waajiri 3,000 na wahitimu 8,000 kutoka katika sekta mbalimbali ambao walitupatia data muhimu kuhusiana na mahitaji ya soko la ajira na nafasi ya wahitimu wetu katika soko hilo", amesema Prof. Anangisye.

Prof. Masoud Muruke, ambaye ni Mratibu wa Mapitio ya Mitaala chini ya Mradi wa HEET-UDSM amesema kwamba hatua ya awali kabisa ya mchakato ilikuwa ni kuhusishwa kwa Kamati za Ushauri tofauti na ilivyozoeleka.

"Kamati hizi zinajumuisha wataalamu kutoka katika tasnia mbalimbali pamoja na wanataaluma ambao kwa pamoja wametoa maarifa muhimu sana kulingana na hali halisi ya soko la ajira, ujuzi unaohitajika na teknolojia zinazoibuka. Michango yao imetusaidia kuhakikisha kuwa wahitimu wa UDSM wanakuwa na ujuzi na maarifa yanayohitajika na hivyo kuwawezesha kufanya vyema katika utekelezaji wa majukumu yao baada ya kuhitimu", amesema Prof. Muruke.

Ameongezea kuwa, "matokeo ya utafiti fuatizi, pamoja na ulinganishi viwango uliofanywa ndani na nje ya bara la Afrika vimekuwa na mchango mkubwa sana katika mchakato wa mapitio ya mitaala. Ushirikishwaji wa Kamati za Ushauri ni ishara muhimu kuwa kuna hatua iliyopigwa katika utekelezaji wa mipango mbalimbali. Jitihada za ushirikishwaji wa wataalamu wa sekta mbalimbali kunazifanya programu zetu za kitaaluma kuendana na mahitaji na viwango vinavyotakiwa".

Prof. Muruke ameeleza zaidi kwamba, matunda ya jitihada hizi shirikishi zilizofanywa ni kuandaliwa kwa mwongozo wa mbinu bunifu za ufundishaji. "Mwongozo huu, ambao upo katika mchakato wa kuidhinishwa utakuwa kielelezo muhimu kwa wanataaluma katika kuhakikisha kwamba mitaala iliyopitiwa inafundishwa kwa namna ambayo inaendana na viwango vinavyokubalika kimataifa".

***Inaendele Uk 19...***

# Mradi wa HEET Wafanikisha Kupatikana kwa Vifaa vya Kisasa vya Mawasiliano UDSM

*Na Jackson Isdory na Wilson Remmy, UDSM-HEET*



Maofisa wa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko (CMU) cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakiongozwa na Mkuu wa Kitengo hicho, Dkt. Dotto Paul Kuhenga (wa nne kutoka kulia, waliosimama) wakiwa na baadhi ya wafanyakazi wa Taasisi ya Sayansi za Baharini (IMS), Zanzibar wakiongozwa na Mkurugenzi wa IMS, Dkt. Magreth Kyewalyanga (wa tatu kulia, waliosimama) wakati CMU ilipotembelea IMS hivi karibuni






Katika jitihada za kuimarisha mawasiliano na uhusiano kwa umma, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kupitia Mradi wa HEET kimenunua vifaa vya kisasa vya mawasiliano kwa lengo la kutangaza shughuli zake na za Mradi.

Akizungumza wakati wa kukabidhi vifaa hivyo kwa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko, Prof. Bernadeta Killian, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo-Mipango, Fedha na Utawala na Mratibu wa HEET-UDSM, alisisitiza umuhimu wa vifaa hivyo vya kisasa katika kutimiza azma ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ya kuimarisha mawasiliano yake na umma kwa kutumia teknolojia ya kisasa.

Prof. Killian ameendelea kueleza kwamba, kadiri Mradi wa HEET UDSM unavyoendelea kutekelezwa, ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya kisasa vya mawasiliano, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinaahidi kujiimarisha katika utoaji wa habari kuhusu Mradi na kuleta mabadiliko katika uga wa kitaaluma na maeneo mengine.

Amesisitiza kwamba, Menejimenti ya Chuo inaamini kwamba vifaa hivyo vitatumika vizuri na kwa manufaa mapana ya kitaasisi. “Ni muhimu sana kwa watumiaji wa vifaa hivi kuvitunza kwa umakini ili kuhakikisha kwamba vinadumu na kuleta ufanisi wa kitaasisi”.

Miongoni mwa vifaa vilivyonunuliwa ni pamoja na kamera zenye ubora wa hali ya juu na vifaa vya kisasa vya kusikilizia. Vifaa vyote hivi vinatumia zana za kisasa ambapo kwa pamoja vitaboresha mkakati wa kukusanya habari kwa ufanisi na kuandaa taarifa zenye ubora kwa ajili ya kuzisambaza katika jamii.

Dkt. Dotto Paul Kuhenga, Mratibu wa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko, UDSM na Mtaalamu wa Uhusiano kwa Umma wa Mradi wa HEET, aliupongeza uwekezaji huo ikiwa ni kielelezo bora na dhamira ya dhati ya UDSM kufanikisha mawasiliano ya Mradi wa HEET na ya UDSM kwa ujumla. “Uwekezaji huu unaendana na dhamira yetu ya kuwashirikisha wadau kuhusu hatua mbalimbali zinaoendelea kuhusu Mradi wa HEET na mipango ya UDSM kwa ujumla”.

“Tunaishukuru Menejimenti ya Chuo na uongozi wa Mradi wa HEET kwa kutambua kitengo cha Mawasiliano kama moja ya maeneo muhimu ya kunufaika na Mradi na kufanikisha hatua mbalimbali za utekelezaji wa Mradi. Tunaahidi kuzingatia matumizi sahihi ya teknolojia na vifaa vya kisasa vilivyonunuliwa ili kuhakikisha kuwa wadau wetu wanapata taarifa kuhusu hatua mbalimbali za utekelezaji wa Mradi na mipango ya Chuo kwa ujumla”, amesema Dkt. Kuhenga.

Bi. Zamda George, Afisa Biashara na Masoko, alisisitiza umuhimu wa masimulizi na shuhuda mbalimbali na athari zake katika kuujulisha umma kuhusu uendeshaji wa Mradi na mipango ya Chuo kwa ujumla. “Uwekezaji huu wa kimkakati sio tu kwamba unatupatia vitendea kazi bali pia unakiweka Chuo katika nafasi nzuri ya kujitangaza katika ulimwengu wa kitaaluma kwa kutumia vifaa vya kisasa kiteknolojia”.











*Baadhi ya wafanyakazi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakiwa katika moja ya mafunzo kuhusu jinsia na kuimarisha ujumuishaji.*

# Mkakati wa Kuzuia Ukatili wa Kijinsia Waimarishwa Kupitia Mradi wa HEET

Na Zamda George, UDSM-HEET

Wakati Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kikiendelea kuwa kinara katika kukabiliana na ukatili wa kijinsia na kuimarisha ujumuishaji, ni dhahiri kuwa jitihada hizo zimeimarishwa na Mradi unaofadhiliwa na HEET.

Akizungumza wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika UDSM, Tarehe 7 Machi 2024, Prof. Bonaventure Rutinwa, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo-Taaluma, alisema, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinathamini jitihada mbalimbali ambazo zimekuwa zikifanywa na vitengo vyake husika na Mradi wa HEET katika kuleta usawa wa kijinsia, ikiwa ni pamoja na kuanzisha sera na taratibu mpya kama vile Mkakati wa Haki Sawa za Kijinsia wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

"Uundaji wa sera mbalimbali za kuzuia ukatili wa kijinsia na uzinduzi wa Dawati la Jinsia la UDSM unaonesha dhamira yetu ya kuzuia ukatili wa kijinsia na matukio ya unyanyasaji wa kingono miongoni mwa wanafunzi na wafanyakazi", amesema Prof. Rutinwa.

Kwa mujibu wa Dkt. Liberato Haule, Naibu Mratibu wa HEET UDSM, Mradi wa HEET ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, umekuwa chachu ya maendeleo makubwa katika kukuza mazingira salama na yenye usawa wa kitaaluma katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Dkt. Haule aliangazia mipango ya kimkakati ya HEET inayolenga kuimarisha usawa wa kijinsia na kuzuia unyanyasaji wa kijinsia ndani ya jumuiya ya chuo kikuu na kusisitiza jukumu muhimu la wanawake katika maendeleo ya taifa.

"Uandaaji wa miongozo na sera za kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia na ukatili wa kingono umekuwa miongoni mwa shughuli muhimu katika mradi. Hii inaonesha dhamira ya Chuo na lengo la Mradi wa HEET katika kujenga mazingira salama na faafu kwa wanafunzi na wafanyakazi wote", amesema Dkt. Haule.

Prof. Nelson Boniface, Kaimu Naibu Makamu Mkuu wa Chuo- Utafiti, alitaja mipango na sera mbalimbali za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam zilizoundwa kwa lengo la kuwawezesha wanawake; kama vile, ufadhili unaozingatia ufaulu wa kitaaluma, fursa za maendeleo ya kitaaluma, na kusaidia wasichana kusoma masomo ya Sayansi, Teknolojia, na Hisabati.

Alieleza pia kuhusu juhudi za Chuo katika kupambana na ukatili wa kijinsia na kukuza utamaduni wa heshima na usalama kupitia miongozo iliyowekwa ya namna ya kushughulikia malalamiko.

Naye Mkurugenzi wa Taasisi ya Taaluma za Jinsia ambaye pia ni Mtaalamu wa masuala ya Jinsia na Mahitaji Maalumu katika Mradi wa HEET-UDSM, Dkt. Lulu Mahai ametoa shukrani kwa washiriki wote kwa kujitolea kwao katika kuhamasisha usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake.

Ameendelea kusisitiza juu ya umuhimu wa mipango inayoangaziwa katika Mradi wa HEET katika kuleta mabadiliko chanya na kuimarisha mazingira jumuishi ya kitaaluma. Ameeleza pia umuhimu wa kuwa na fursa sawa ya ustawi na kusisitiza kuhusu mkakati wa Chuo katika kushughulikia masuala ya kijinsia kwa weledi wa hali ya juu.

# Mwongozo wa Kushughulikia Malalamiko Maeneo ya Ujenzi Waandaliwa

*Na Mercy Machange, UDSM-HEET*



Mtaalamu wa masuala ya Jamii katika Mradi wa HEET-UDSM, Dkt. Jacquline Mgumia (aliyesimama) akizungumza na baadhi wa wadau juu ya utoaji wa maoni na malalamiko kuhusu mradi wa HEET, Chuoni hivi karibuni.



Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinachukua hatua zote stahiki kuhakikisha kwamba kunakuwa na ufanisi katika utekelezaji wa Mradi wa HEET kwa kuimarisha na kuandaa Mwongozo wa Kushughulikia Malalamiko katika maeneo ya ujenzi.

Taarifa zilizoelezwa na Naibu Mratibu wa HEET-UDSM, Dkt. Liberato Haule, zinaonesha kuwa ujenzi wa majengo 24 ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam unaendelea katika maeneo mbalimbali ya Mradi wa HEET, kufuatia utiaji saini wa mikataba na wakandarasi wanne hivi karibuni.

Maeneo hayo yapo katika Mkoa wa Dar es Salaam, Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere-Mlimani, Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia, Ndaki ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Shule Kuu ya Sayansi Akua na Teknolojia ya Uvuvi, Kunduchi; Zanzibar -Taasisi ya Sayansi za Bahari. Aidha, maeneo mengine ni Kampasi za Lindi na Kagera.

Akizungumza na Jarida hili hivi karibuni, Mtaalamu wa Maendeleo ya Jamii HEET-UDSM, Dkt. Jacqueline Mgumia, amesema kuwa mpango wa kujumuisha Mwongozo wa Kushughulikia Malalamiko katika maeneo ya ujenzi umeonesha dhamira ya UDSM ya kushughulikia malalamiko kwa mujibu wa mahitaji ya Mfumo wa Mazingira na Jamii (ESF) kama yanavyobainishwa na Serikali na Benki ya Dunia.

"Mwongozo wa Kushughulikia Malalamiko una jukumu muhimu la kushughulikia malalamiko yanayotolewa na watu walioathiriwa na mradi, kuwapa njia rasmi ya kuwasilisha malalamiko au kutoa maoni kuhusu utekelezaji wa mradi. Kwa kutambua umuhimu huu, Chuo kimeandaa Mwongozo wa Kushughulikia Malalamiko katika hatua mbalimbali ili kuwezesha utatuzi wa haraka na wa uwazi wa malalamiko", amesema Dkt. Mgumia.

Ameendelea kueleza kuwa katika ngazi ya ujenzi, Kamati teule za Kushughulikia Malalamiko katika eneo la ujenzi ziliundwa zikijumuisha wawakilishi kutoka taasisi zinazotekeleza mradi, wakandarasi wa ujenzi, wanafunzi na maafisa husika wa serikali za mitaa husika.

"Kamati hizi zina jukumu la kushughulikia kwa haraka malalamiko yanayohusiana na shughuli za maendeleo ya ujenzi. Maafisa wa kushughulikia malalamiko wameteuliwa kufanikisha ushughulikiaji wa malalamiko na kutunza kumbukumbu na utatuzi wa malalamiko", amesema Dkt. Mgumia.

*inaendelea uk. 19...*



# Ushughulikiaji wa Malalamiko.........

kutoka uk. 18

## Utatuzi wa Malalamiko

Wakati huohuo, Mtaalamu wa Maendeleo ya Mazingira wa UDSM, Dkt. Edmund Mabhuye, ameeleza kuwa ikiwa kuna malalamiko ambayo hayawezi kutatuliwa katika ngazi ya ujenzi, yanapaswa kuwasilishwa katika ngazi za juu za uamuzi.

"Kitengo cha Utekelezaji wa Mradi wa HEET kitatekeleza jukumu la kushughulikia malalamiko ambayo hayajatatuliwa kwa njia ya haki na inayokubalika. Wadau wana fursa ya kukata rufaa kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ikiwa hawataridhika na utatuzi uliotolewa na Kitengo cha Utekelezaji wa Mradi", amesema Dkt. Mabhuye.

"Kamati hii imeundwa kwa lengo la kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika kushughulikia malalamiko, hatimaye kuboresha mazingira mazuri ya utekelezaji wa mradi", amesema Dkt. Mabhuye.

Ameendelea kueleza kwamba, malalamiko ya kiutendaji yanayotokana na shughuli za taasisi pia yatashughulikiwa kupitia maafisa wa kushughulikia malalamiko walioteuliwa katika ngazi ya Chuo Kikuu, Ndaki na wakala. Maafisa hawa watatunza rekodi za malalamiko na kuhakikisha utatuzi unafanywa kwa wakati na kwa kutumia utaratibu rahisi wa kushughulikia malalamiko.

## Msisitizo Kuhusu Uwazi na Uboreshaji Endelevu

Kwa mujibu wa Dkt. Mabhuye, ili kuongeza uwazi na ufanisi, Chuo kinasisitiza umuhimu wa utunzaji wa kumbukumbu na ufuatiliaji ndani ya mfumo wa Mwongozo wa Kushughulikia Malalamiko, na kwamba taarifa za kila mwezi kuhusu idadi ya malalamiko yaliyopokelewa, kutatuliwa, na yaliyosalia zitatolewa ili kupata taswira ya hali halisi kwa lengo la kuendelea kuboresha maeneo yatakayoonekana kuwa na changamoto kwa lengo la kuendelea kufanya uboreshaji.

"Mwongozo wa Kushughulikia Malamiko ni sehemu muhimu ya dhamira yetu ya uwajibikaji katika utekelezaji wa Mradi, kuhakikisha kuwa malalamiko yote ya wadau wote yanashughulikiwa kwa wakati", amesema Dkt. Mabhuye.

Amesisitiza zaidi kuwa kupitia mwongozo huu, Chuo kimelenga kujenga uaminifu na ushirikiano miongoni mwa wadau wa mradi, na hatimaye kuchangia kufanikisha malengo ya Mradi wa HEET.

# Mchakato wa Mapitio ya Programu 222....

kutoka uk. 17

"Kuwapo kwa majukwaa huru ya kupata rasilimali mbalimbali za kielimu, idadi kubwa ya kozi zinazofundishwa kwa njia ya mtandao na mpango wa uanzishwaji wa kampasi maizi, kunaonesha dhamira ya dhati ya UDSM katika matumizi ya teknolojia za kisasa katika mfumo mzima wa elimu hapa chuoni", amesema Prof. Muruke.

Kupitia Mradi wa HEET na jitihada nyingine zinazofanywa, Chuo kimeanza safari ya mageuzi, ambayo inaonesha mafanikio makubwa katika maendeleo ya kitaaluma na kimiundombinu. Jitihada hizi zinaonesha nia ya dhati ya UDSM katika kukabiliana na changamoto zinazohusiana na uwezo wa programu, udahili wa wanafunzi, na uwiano baina ya hali halisi na ikama.

# Meneja wa Benki ya Dunia Apongeza....

kutoka Uk. 5

## Mapitio ya Mitaala

Wakati huohuo, wadau kutoka katika tasnia mbalimbali wameshuhudia ushirikiano baina yao na UDSM kupitia ofisi ya ushirikiano iliyoanzishwa kupitia Mradi wa HEET.

Dkt. Liberato Haule, Naibu Mratibu wa Mradi wa HEET- UDSM, amesema Chuo kimeandaa miongozo ya ushirikishwaji wa tasnia mbalimbali iliyozingatia maeneo makuu matano.

Ameyataja maeneo hayo kuwa ni: ushirikiano katika shughuli za huduma kwa jamii, uanzishwaji na uendeshaji wa kamati za ushauri, utafiti tumizi, ubunifu na uboreshaji wa miundombinu ya kufundishia, ushirikiano katika mpango wa wafanyakazi waambata na nafasi za mazoezi kwa vitendo na ukurufunzi kwa wanafunzi na wahitimu.



# UDSM Chapiga Hatua Kubwa Utekelezaji wa Mradi wa HEET

Na Dotto Kuhenga, UDSM-HEET



*Mkurugenzi wa Elimu ya Juu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Pof. Peter Msoffe (katikati, waliokaa), Mratibu wa Mradi wa HEET Kitaifa, Dkt. Kenneth Hosea (wa kwanza kulia, waliokaa), Mratibu wa HEET-UDSM, Prof. Bernadeta Killian (wa kwanza kushoto, waliokaa) na wadau kutoka katika sekta, katika moja ya vikao vya mradi wa HEET, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, hivi karibuni.*

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimeripoti hatua muhimu zilizofikiwa katika utekelezaji wa Mradi wa HEET tunapokaribia kufikia mwishoni katika kipengele cha kujenga uwezo na kuanzisha ushirikiano baina ya Chuo na tasnia mbalimbali.


Akizungumza katika mkutano wa waratibu wa Mradi wa HEET uliofanyika jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 26 hadi 28 Februari 2024, Naibu Mratibu wa Mradi wa HEET-UDSM, Dkt. Liberato Haule, ameripoti kuhusu mafanikio makubwa yaliyofikiwa, siyo tu katika maeneo hayo mawili bali pia katika mapitio ya mitaala na mpango wa matumizi ya mbinu bunifu za ufundishaji ambao upo katika hatua ya kuidhinishwa.

Katika mkutano huo ulioandaliwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dkt. Haule alidokeza kuwa, kwa upande wa kuwajengea uwezo watumishi wanataaluma, Chuo kimevuka lengo kwa kutoa ufadhili kwa wanataaluma 23 kwa ajili ya masomo ya shahada za uzamili wanaosoma nje ya nchi ikilinganishwa na mpango uliokuwepo wa kusomesha wanataaluma 22.

“Kwa muktadha huu, ufadhili wa kundi la mwisho la wafanyakazi wanane ulitolewa mwezi Juni 2023 ambapo wanne ni wa uzamivu na wanne ni wa umahiri. Tunafurahi pia kuripoti kwamba wafanyakazi watano ambao walipewa ufadhili wa shahada ya umahiri katika kundi la kwanza tayari wamekamilisha masomo yao na wameripoti kazini”, amesema Dkt. Haule.

Akielezea maendeleo katika kujenga uhusiano wa kiutendaji na sekta au tasnia binafsi, Dkt. Haule amesema kuwa, Chuo kimetekeleza kwa ufanisi takriban shughuli zote zinazohitajika. Miongozo mbalimbali imeandaliwa na kamati tano za ushauri wa kitasnia zimeundwa na kufanya mikutano yao kama ilivyopangwa.

Ameendelea kueleza kuwa, tayari Ofisi ya Ushirikiano imekwishaanzishwa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo Mratibu amekwishateuliwa na kuanza majukumu yake. Aidha, wanataaluma 12 wamekamilisha mikataba yao ya uambata wa wanataaluma kufuatia mikataba mitano iliyosainiwa baina ya UDSM na tasnia mbalimbali.



*inatoka Uk. 20*




## UDSM Chasaini Mikataba ya Ujenzi wa Majengo 21 ya Kisasa

Wakati huohuo, Profesa Bernadeta Killian, Mratibu wa HEET- UDSM na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo-Mipango, Fedha na Utawala, amesema, hivi karibuni UDSM ilisaini mikataba na wakandarasi wanne kwa ajili ya ujenzi wa majengo 21, kati ya 24 yaliyopangwa kujengwa kupitia Mradi wa HEET.

Prof. Killian ambaye pia alimwakilisha Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. William A. L. Anangisye, katika mkutano huo, alisema wakandarasi wanne waliosaini mikataba ya kutekeleza miradi ya ujenzi ni: M/S Mohammed Builders; M/S B.H. Ladwa; M/S Til Construction; and M/S Shandong Hi-Speed.

Alibainisha kuwa, mikataba hiyo itahusu shughuli za ujenzi katika ndaki mbalimbali katika Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere-Mlimani yenye thamani ya TZS 6,643,437,375.37; ujenzi wa majengo mapya 11 yakiwamo: jengo la utawala na jengo la kitaaluma na jengo moja jipya la hosteli kwa wanafunzi 80 katika Taasisi ya Sayansi za Bahari iliyopo Buyu, Zanzibar, wenye thamani ya TZS 10,118,405,530.78; na shughuli za ujenzi zenye thamani ya TZS 13,719,450,687.7 katika maeneo ya Ruangwa na Ngongo mkoani Lindi.

Ameendelea kueleza kuwa, Chuo kilisaini mkataba wa usimamizi na M/s Mhandisi Consultancy Ltd akishirikiana na M/s MD Consultancy Limited na wengine kwa ajili ya kusimamia ujenzi wa majengo matatu katika Kampasi ya Kagera.

Majengo hayo matatu katika kampasi ya Kagera, ambayo yanafanya jumla ya majengo 24 yanayojengwa chini ya Mradi wa HEET katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ni pamoja na: jengo la utawala na jengo la masuala ya kitaaluma, kafteria, jengo la biashara, na jengo la hosteli za wanafunzi wa kike.

Wakati huohuo, Mkurugenzi wa Elimu ya Juu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Peter Msoffe, amesema mkutano huo ulilenga kupokea taarifa za maendeleo ya utekelezaji wa miradi kutoka katika taasisi mbalimbali za wanufaika na kuweka mkakati wa kusonga mbele kwa ajili ya kuboresha zaidi.

"Mkutano huu ni muhimu sana kwa kuwa unatupatia fursa ya kufahamu maendeleo yaliyofikiwa na changamoto ambazo kila taasisi inakabiliwa nazo katika utekelezaji wa mradi. Pia, ni fursa muhimu sana ya kukumbushana kanuni na viwango vya serikali na Benki ya Dunia kwa ajili ya kuzingatiwa wakati wa utekelezaji wa Mradi huu.", amesema Prof. Msoffe.

## Maeneo ya Vipaumbele katika Mradi wa HEET- UDSM

Kwa ujumla wake, Mradi wa HEET wa Dola za Marekani milioni 47.5 kwa UDSM unazingatia maeneo manane muhimu, ambayo ni: ujenzi na ukarabati wa miundombinu; mapitio ya mitaala na mpango wa mbinu bunifu katika ufundishaji na uimarishaji wa masuala ya utafiti tumizi na ubunifu.

Maeneo mengine ni pamoja na: uanzishwaji wa ushirikiano baina ya Chuo na tasnia ya uhusiano wa kazi na sekta/ tasnia binafsi, kuimarisha matumizi ya teknolojia ya dijitali, kukuza uwezo wa ndani wa kuzalisha mapato, kujenga uwezo wa wanataaluma na uongozi wa chuo pamoja na usimamizi, uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya Mradi.














*Bw. Vicent Faustine Tsoray, Mhitimu wa Shahada ya Umahiri ya Sayansi katika Mustakabali Endelevu wa Chakula, Chuo Kikuu cha Cranfield, nchini Uingereza.*

# Mnufaika Mwingine Kupitia Mradi wa HEET- UDSM Ahitimu Masomo ya Umahiri

*Na Ally Mambele, HEET-UDSM*

Mwanataaluma mmoja wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambaye ni miongoni mwa wanufaika wa ufadhili wa elimu ya juu uliotolewa na Mradi wa HEET, Bw. Vicent Faustine Tsoray, amefanikiwa kuhitimu masomo ya umahiri hivi karibuni, Jarida hili linaripoti.

Bwana Tsoray sasa anajiunga na kundi la kwanza la wanataaluma wengine wanne ambao ni wanufaika wa HEET ambao walihitimu masomo yao ya umahiri mwishoni mwa mwaka jana, 2023.

Bw. Tsoray, Mkufunzi Msaidizi katika Idara ya Uhandisi wa Kilimo, Ndaki ya Kilimo na Teknolojia ya Chakula, alikamilisha shahada yake ya Umahiri ya Sayansi katika Mustakabali Endelevu wa Chakula katika Chuo Kikuu cha Cranfield, Uingereza.

"Ufadhili huu ulikuwa chini ya bajeti ya UDSM USIP, na sehemu ya ruzuku ya Dola za Kimarekani 200,000 kwa ajili ya mafunzo ya muda mrefu iliyotolewa chini ya Mradi wa HEET. Tunafurahi kuona kwamba mpaka sasa tuna wanataaluma watano ambao wamemaliza masomo yao kwa mafanikio", amesema Dkt. Stephen Matee, Mtaalamu wa Kujenga Uwezo wa Mradi wa HEET-UDSM.

Kwa mujibu wa Dkt. Matee, Bw. Tsoray ni miongoni mwa watumishi kumi wa UDSM waliojisajili kwa ajili ya masomo katika ngazi ya umahiri chini ya ufadhili wa HEET-UDSM. "Tunafurahi kuripoti kwamba kufikia Aprili, 2024, wanataaluma watano kati ya hawa kumi waliopata ufadhili wa Mradi wamekamilisha masomo yao kwa mafanikio".

Dkt. Matee aliendelea kusema kuwa, kwa upande wa ufadhili wa HEET-UDSM tayari kimevuka lengo kutoka kutoa udhamini wa masomo kwa wanataaluma 22 hadi 23 ambapo, kati yao 10 ni wa masomo ya umahiri na 13 ni wa masomo ya uzamivu.

Wakati huohuo, Bw. Tsoray alitoa shukrani zake za dhati kwa timu ya Mradi wa HEET-UDSM na wale wote waliochangia katika kufanikisha ufadhili huo. "Kwa kweli ninahisi kuwajibika kwa kutumia maarifa na ujuzi niliopata kwa manufaa ya jamii na kufanikisha malengo ya Mradi wa HEET"

## Wanufaika 4 wa ufadhili katika Programu ya MSC Wahitimu 2023

Mwezi Novemba 2023, Jarida hili liliripoti kuwa wafanyakazi wanne waliojisajili katika ngazi ya umahiri chini ya ufadhili wa Mradi wa HEET-UDSM wamefanikiwa kukamilisha masomo yao nje ya nchi na kurudi kituo chao cha kazi, UDSM, kuendelea na majukumu.

Wanataaluma hao wanne wanatoka Ndaki ya Kilimo na Teknolojia ya Chakula pamoja na Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia. Wanataaluma hao ni: Bi. Angelina William Mwakosya, Bi. Salma Damla, Bw. Gabriel Mwaijande Paul na Bi. Mariam Madundo.

Bi. Angelina William, Mkufunzi Msaidizi, kutoka Idara ya Sayansi ya Chakula katika Ndaki ya Kilimo na Teknolojia ya Chakula, CoAF, alipata ufadhili wa HEET mwezi Julai, 2022 kwa ajili ya masomo ya umahiri katika Sayansi ya Chakula katika Chuo Kikuu cha Reading, Uingereza. Bi. Angelina William alitoa shukrani zake za dhati kwa fursa muhimu aliyopatawa kupitia Mradi wa HEET.

Mfanyakazi mwingine ni Bi. Salma Damla, Mkufunzi Msaidizi kutoka Idara ya Sayansi ya Chakula, Ndaki ya Kilimo na Teknolojia ya Chakula. Bi. Salma Damla aliyekamilisha shahada ya umahiri katika Chuo Kikuu cha Leeds, Uingereza, pia alitoa shukrani zake za dhati kwa fursa hiyo.

Wengine ni: Bw. Gabriel Mwaijande Paul, kutoka Idara ya Uhandisi wa Usafirishaji na Jiotekniki na Uhandisi wa Kijiolojia, Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia, ambaye alimaliza shahada yake ya umahiri katika Uhandisi Jiotekniki kutoka katika Chuo Kikuu cha Leeds, Uingereza na Bi. Mariam Madundo, kutoka Idara ya Uhandisi Mihimili na Ujenzi, Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia ambao nao walishukuru kwa ufadhili huo.

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

HEET
HIGHER EDUCATION FOR ECONOMIC TRANSFORMATION

## Mawasiliano


Naibu Mratibu: +255 765 939 958

Mhariri Mkuu: +255 755 172 570

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam,
Jengo la Cranford Pratt,
Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere, Mlimani
Barabara ya Chuo Kikuu, 16103 Ubungo
S.L.P. 35091
Dar es Salaam, Tanzania

heet@udsm.ac.tz Heet Udsm www.udsm.ac.tz